

MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA TAREHE 20/10/2021 KATIKA OFISI YA KITENGO CHA MANUNUZI HALMASHAURI YA WILAYA YA KONGWA - KUPITIA NA KUJADILI UJENZI WA MADARASA, BWENI, JENGO LA DHARURA NA NYUMBA YA WATUMISHI MIRADI YA UVIKO 19

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA:**

NA.	JINA	CHEO
1.	Hamisi Sombwe	Mwenyekiti
2.	Praygod G. Munisi	Katibu
3.	Paskalina Duwe	Mjumbe
4.	Eugen Shirima	Mjumbe
5.	Eng.Amina Msangi	Mjumbe
6.	Ben Kigoma	Mwalikwa wa kudumu

**T-BODI/KOG/2021-2022/1: KUFUNGUA KIKAO:**

Mwenyekiti alifungua kikao saa 13.30 mchana kwa kuwakaribisha wajumbe na kuwaomba ushiriki wenye tija katika zoezi zima la kupitia na kuzijadili kwa kina agenda za kikao.

**T-BODI/KOG/2021-2022/2: KUSOMA NA KUDHIBITISHA AGENDA:**

Katibu aliwasilisha agenda zifuatazo katika kikao hicho kwa ridhaa ya Mwenyekiti.

- Kufungua kikao
- Kuthibitisha agenda
- Kupitia na kujadili ujenzi wa madarasa, bwani, jengo la dharura na nyumba ya watumishi miradi ya Uviko 19
- Kufunga kikao

Wajumbe walizipokea, walizipitia na kuridhia agenda zote kuwa agenda halali za kikao.

**T-BODI/KOG/2021-2022/3: KUPITIA NA KUJADILI UJENZI WA MADARASA, BWENI, JENGO LA DHARURA NA NYUMBA YA WATUMISHI MIRADI YA UVIKO 19**

Wajumbe walipewa taarifa kuwa Halmashauri imepokea fedha kwa ajili ya ujenzi wa madarasa ya shule za sekondari na shule shikizi za msingi, bwani moja la shule ya msingi, ujenzi wa jengo la dharura na nyumba tatu kwa moja za watumishi katika Idara ya Afya ambazo zitagharimu Tshs 3,070,000,000/=

Kwa mchanganuo ufuatao;

Madarasa shule za sekondari na Msingi  $130 @ 20,000,000 = 2,600,000,000$

Jengo la Dharura Tshs 300,000,000

Nyumba za watumishi tatu kwa moja 90,000,000  
Bweni 80,000,000

Wajumbe walipokea taarifa na kuidhinisha matumizi ya fedha hizo kwa kazi iliyokusudia na kuidhinisha kutumia utaratibu wa force account na Njia ya manunuzi ya chanzo kimoja. Msisitizo ulitolewa na wajumbe kuwa dhamani ya fedha ionekane katika miradi itakayotekelezwa.

**T-BODI/KOG/2021-2022/4: KUFUNGA KIKAO.**

Mwenyekiti alifunga kikao mnamo saa 15.32 mchana kwa kuwashukuru wajumbe waliohudhuria kikao hicho.



MWENYEKITI

UMETHIBITISHWA



KATIBU

20/10/2021  
TAREHE